

# HADITHI QUDSI

Kimetarjumiwa na:  
**Zakirhusein Muhammad Lakha**

Kimehaririwa na:  
**Ramadhani Kanju Shemahimbo**

# YALIYOMO

## **Sura ya 1**

Kwa hakika kifo kitagonga mlango (kitafika tu).....2

## **Sura ya 2**

Kujikurubisha kwa Allah (s.w.t).....3

## **Sura ya 3**

Tuungane na nafsi (roho) zilizopata utulivu.....5

## **Sura ya 4**

Allah (s.w.t) anasema.....6

## **Sura ya 5**

Vitendo vyema hujieleza zaidi kuliko maneno.....7

## **Sura ya 6**

Usafishe moyo wako dhidi ya kuipenda dunia.....8

Vitendo vyema vitano vitang'arisha kaburi lako.....9

## **Sura ya 7**

Binadamu ameumbwa kwa ajili ya lengo adhim.....10

## **Sura ya 8**

Wanadamu kwa sababu gani nyiyi hamzilindi nafsi zenu dhidi ya ghadhabu ya Mungu wenu?.....11

## **Sura ya 9**

Hakuna mmoja aliyekuwa mbora kuliko mwenzi.....12

## **Sura ya 10**

Kwa hakika binaadamu ameidhulumu nafsi yake.....14

## **Sura ya 11**

Yule anayemdhalilisha mwenye imani.....14

## **Sura ya 12**

Kila kitu kitaangamia ila Mwenyezi Mungu.....16

## **Sura ya 13**

Jiendeleze kwa ajili yangu (Allah) na jifurahishe kwa neema zangu.....17

## **Sura ya 14**

Uislamu ulio hai.....18

## **Sura ya 15**

Nitii mimi ili uweze kuwa na uwezo kama mimi .....20

## **Sura ya 16**

Mpaka lini wewe binadamu utatengana na mimi (Allah s.w.t).....21

## **Sura ya 17**

Niite, Nami nitakuitikia.....23

## **Sura ya 18**

Hakuna hekima bila kutafakari.....24

## **Sura ya 19**

Kwa hakika kifo kitafichua vitendo vyako.....25

## **Sura ya 20**

Bila shaka wakati wa kutoa hesabu uko karibu.....27

## **Sura ya 21**

Kuangamia kwako hutokana na ulimi wako.....28

## **Sura ya 22**

Na mimi ni Bwana Mungu wako wewe unitambue.....29

## **Sura ya 23**

Bishara njema zilizotangazwa kwa ajili ya watu watakaoenda  
Peponi.....30

## **Sura ya 24**

Uwe kwa ajili yangu na mimi nitakuwa kwa ajili yako.....32

## **Sura ya 25**

Jilinde na jihurumie nafsi yako dhidi ya moto wa Jahannam.....33

## **Sura ya 26**

Zawadi ya milele kwa ajili ya watenda mema.....35

## **Sura ya 27**

Kuwa Mnyenyeketu ili unijue mimi (Allah s.w.t) ujipatie maarifa juu  
yangu.....38

## **Sura ya 28**

Uwe unajali faradhi yako kuhusu Mungu wako.....39

## **Sura ya 29**

Nikumbuke mimi kwa dhati na kwa nia.....40

## **Sura ya 30**

Nikumbuke mimi kwa kudumu (kuomba toba kwa kulia na masikitiko) na

mimi Allah (s.w.t.). Nitakukumbuka kwa kukuhurumia.....42

### **Sura ya 31**

Akhera Pepo yangu. Inazidi dhara dunia .....43

### **Sura ya 32**

Anayenitafuta mimi (Allah) Basi atanipata.....44

### **Sura ya 33**

Mimi nayajua yaliyojificha moyoni mwako.....46

### **Sura ya 34**

Ee Mwanadamu usidanganyike na kimeto na mtua wa dunia.....47

### **Sura ya 35**

Kuwa na huruma na mkarimu kwa wengine.....49

### **Sura ya 36**

Kama upendavyo kwa ajili yako, basi upende hivyo hivyo kwa ajili ya wengine.....50

### **Sura ya 37**

Usijionyeshe.....52

### **Sura ya 38**

Ee Mwanadamu wewe ni kiumbe mdhoofu na mmi bwana Mtukufu na mwenye uwezo wote.....53

### **Sura ya 39**

Hii dunia ni burudani na mchezo.....55

## DIBAJI

### Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Mwenye kurehemu

Sifa zote njema anastahiki Allah (s.w.t.) aliyeumba ulimwengu na kusimamisha mbingu bila nguzo, kwa hakika yeye husikiliza dua zetu tuanazosoma na husikiliza hata tukimtaja kwa siri. Yeye ndiye anayetangua mateso, misiba, kuondosha kiza, kutakasa miyo yetu. Kwa kupitia rehema, hujalia matumaini kwa wale waliokata tamaa. Yeye hudhihirisha ukarimu wake ambao hauna mfano na kuwalalia riziki binadamu kupita kiwango kinachohitajika.

Salam ziwe kwa mitume yake yote aliyotutumia pamoja na maimamu wa haki aliowatakasa na khasa kwa mpenzi wake Muhammad Al-Mustafa (s.a.w.) ambaye ni lakiri wa mitume. Hakika ni neema kubwa mno ya Allah (s.w.t.) licha ya kutufundisha namna ya kumomba yeye lakini vile vile hata namna ya kuzungumza na yeye kupitia dua.

Kupitia hizo dua mtu hugundua kuna ruwaza ya ukarimu na wema. Ikiwa binadamu atatengana na silisili (pattern) zilizo pandikizwa na waovu, basi kwa hakika binadamu amejaliwa uwezo kujiokoa nafsi yake kutoptana na khofu inayomkabili katika maisha yake ya kila siku, hiyo itaweza kumgeuza binadamu kuwa kiumbe mtiifu na mwabudu wa Allah (s.w.t.) tu ambalo ndio lengo la kuumbwa kwake.




Hizi Hadith Al-Qudsi ni tarjuma ya kitabu *Al-hadith al-qudsi* kilichotarjumiwa na ndugu N. M. Walji wa Nairobi chini ya uangalizi wa Seyyid Murtadha M. Murtadha.


Tunamuomba Allah (s.w.t.), kuitia Mtume wetu Muhammad (s.a.w.) ambaye ni rehma wa walimwengu pamoja na Ahlul-Bayt wake waliyotakaswa, atukubalie amali zetu (Amin).

**Zakirhusein Muhamed Lakha**  
**S.L.P. 11361**  
**Arusha**  
**Tanzania**  
Barua pepe: [hussein\\_zakir@yahoo.com](mailto:hussein_zakir@yahoo.com)

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ







## **Hadithi Qudsi**

### **SURA YA 1**

#### **KWA HAKIKA KIFO KITAGONGA MLANGO (KITAFIKA TU)**

##### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Mimi ninashangazwa na mtu ambaye ana hakika ya kufa, vipi anafurahi.
2. Mimi ninashangazwa na mtu huyo, ana hakika ya siku ya kutoa hesabu ‘Qiyama,’ lakini huendelea kukusanya mali.
3. Mimi ninashangazwa na huyo mtu mwenye hakika ya kuingizwa kaburini lakini hutabasamu na kutojishughilisha.
4. Mimi ninashangazwa na huyo mtu ana hakika ya kuangamia kwa dunia lakini hutabasamu utulivu kwayo kwa kuipenda.
5. Mimi nashngazwa na huyo mtu ambaye maneno yake yamejaa hekima lakini moyo wake umejaa ujinga.
6. Mimi nashangazwa na mtu ambaye ana yakini ya kubakia kwa Akhera na neema zake vipi anastarehe.
7. Mimi ninashangazwa na mtu anayejisafisha kwa maji, lakini moyo wake si safi.
8. Mimi ninashagazwa na mtu huyo, huchunguza aibu za wenzake; lakini husahau aibu zake.

## **Hadithi Qudsi**

9. Mimi ninashangazwa na huyo mtu ambaye anajua kwamba Allah (s.w.t) Anajua vitendo vyake lakini huendelea kumuasi.
10. Mimi ninashangazwa na huyo mtu huhubiria watu wengine lakini haihubirii nafsi yake. (Kutosahihisha nafsi yake).
11. Mimi ninashangazwa na huyo mtu anayejua kwamba atakufa, kulazwa kaburini peke yake, lakini huendelea kujishughulisha mno na watu ambao hawataweza kumsaidia.  
Allah (s.w.t.) anasema: "Hakuna Mungu ila Mimi, na Muhammad ni Mtumishi wangu."
12. Mimi ninashangazwa na huyo mtu mwenye uhakika wa Akhera na neema zake lakini hajishughulishi kuzipata.

## **SURA YA 2**

### **KUJIKURUBISHA KWA ALLAH (S.W.T.).**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Ushahidi Muhimu wa kuwepo Kwangu ni kwamba hakuna Mungu ila Mimi (Allah) peke yangu bila mshiriki ye yote na Muhammad (s.a.w.) Ni mtumishi na Mjumbe wangu.
2. Mtu asiyefurahishwa na maagizo Yangu, kutokuwa na subra kutokana na majaribio Yangu, kutonishukuru kwa ukarimu Wangu, kutotosheka na neema Zangu, basi amtafute Mola mwine badala yangu na aache ulimwengu Wangu.

## **Hadithi Qudsi**

---

3. Mtu asiyepata anachokitaka hapa duniani, na huhuzunika kwa kukosa ni sawa na kunikasirikia.
4. Yeyote anayelalamika misiba inayomkabili, kwa mtu mwingine ni sawa ya kunishitaki Mimi.
5. Yeyote anayeenda kwa tajiri na kujidhalilisha kutokana na utajiri wake, hupoteza thuluthi moja ya imani yake.
6. Yeyote anayejipiga makofi mbele ya maiti (kutokana na kifo cha mtu huyo) ni sawa na kuchukua upanga kupigana na Mimi (Allah), na mwenye kuvunja kijiti kaburi la maiti ni sawa kabomoa Al-Ka'aba yangu kwa mikono yake.
7. Yeyote asiyejali nini anachokula (kikiwa haramu au halali) basi Mimi sitamjali kumpitisha mlango wowote wa kumuingiza Jahannam.
8. Yeyote asiyejaribu kuboresha imani yake (kwa kutenda vitendo vyema) yumo katika hasara. Yeyote aliyomo katika hasara basi kifo ni bora kwa ajili yake.
9. Yeyote atayejaribu kuishi maisha kutokana na maarifa yake, basi Mimi nitamwongezea maarifa juu ya maarifa na kutambua vitendo vyake.

## **Hadithi Qudsi**

# **SURA YA 3**

### **TUUNGANE NA NAFSI (ROHO) ZILIZOPATA UTULIVU**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Ee Mwanaadam! Yeyote aliyetosheka basi mtu huyo ni tajiri. Na mwenye kuridhia na kichache duniani basi amemtegemea Mungu Mtukufu.
2. Yeyote asiye na uvivu basi hupata utulivu.
3. Mwenye kuacha husuda amestarehe, na anayejiепusha na mambo ya haramu ametakasa imani yake.
4. Yeyote asiye na tabia ya umbeya (udaku) hupendwa na watu.
5. Yeyote atatyejitenga na watu basi atasalimika na shari zao.
6. Yeyote anayepunguza kusema (kuzungumza) huongezeka hekima yake.
7. Yeyote anayeridhika na chochote kidogo alichoruzukiwa na Mwenye Enzi Mungu basi Allah huridhika na uchache wa amali yake.
8. Ee Mwanaadam! Wewe huishi na maarifa uliyojaliwa. Basi vii utakuwa mtafutaji wa hekima wakati hutumii maarifa katika uhai wako.

## **Hadithi Qudsi**

10. Ee Mwanaadam! Ikiwa umemaliza uhai wako wote kutafuta mali, basi lini utatafuta maisha ya badaye (Akhera).

## **SURA YA 4**

### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Ee Mwanadam! Mtu yejote anayeanza siku yake kwa uroho na kuipupia dunia, basi huzidi kuwa mbali na Allah (S.W.T.) na hajibidiishi kwa ajili Akhera ila huongeza taabu na ugumu, basi Allah (S.W.T.) huujalia moyo wake pupa isiyoisha, ufukara usio na mwisho abadan, na matarajio asiyoweza kufikia aslan.
2. Ee Mwanadam! Kila siku umri wako hupungua; lakini wewe hutambui. Mimi (Allah) kila siku hukuteremshea riziki, baraka Zangu lakini wewe hunishukuru. Wewe huridhiki na kidogo una-chojaaliwa wala hutosheki kwa kingi unachopata.
3. Ee Mwanadam! Hakuna siku hupita bila wewe kupata riziki yako kutoka Kwangu; na hakuna usiku hata mmoja kupita bila malaika Wangu kuniletea hisabu ya vitendo vyako viovu.
4. Wewe hula riziki Yangu (kutoka Kwangu) na unaniasi, lakini unaponiomba Mimi hukuitikia.
5. Kheri zangu hukushukia, na maasi yako hunijia kila siku. Angalia nilivyo Mola Mwema na ulivyo mja muovu.
6. Mimi (Allah) hukupatia chochote unachoniomba, lakini wewe huendelea kutenda dhambi. Mimi huvisitiri vitendo viovu kimoja

## **Hadithi Qudsi**

baada ya kingine. Mimi Huaibishwa na wewe lakini wewe hunionei haya.

7. Wewe hunisahau Mimi; lakini Mimi, ninakukumbuka wewe. Wewe huwaogopa watu na kutonijali Mimi. Wewe huogopa uadui wao; lakini huogopi ghadhabu Yangu.

## **SURA YA 5**

### **VITENDO VYEMA HUJIELEZA ZAIDI KULIKO MANENO**

**ALLAH (S.W.T.) ANASEMA: EE MWANAADAM! USIWE  
MMOJA WA WAFUATAO:**

1. Wale wanaoomba msamaha kutoka kwenye matarajio yasiyokuwa na kikomo.
2. Wanatumai Pepo lakini hawatenda vitendo vyema vyta kuwafanya wastahiki.
3. Huzungumza kama wacha Mungu, lakini huishi maisha ya kinafiki (kama wanafiki).
4. Wale ambao wamejaaliwa mali lakini hawatosheki.
5. Na wale wasiyojaaliwa kutokuwa na subra.
6. Wale wenye kuamuru mema lakini hawayatendi.
7. Wale wanaoshauri kujiepusha na maovu; lakini hawajiepushi na

## **Hadithi Qudsi**

maovu.

8. Wanaowapenda watu wema, ilihali wao si mionganoni mwao.
9. Wale wanaowachukia wanafiki, lakini wao ni mionganoni mwao.
10. Yule ambaye huwashauri wengine kutenda mema, lakini ye ye hutenda maovu.
11. Ee Mwanaadam! Ardhi daima hulalamika: ‘Wewe hutembea juu yangu, lakini mwishowe utaingia tumboni mwangu. Unafanya maasi juu yangu lakini utaadhibiwa tumboni mwangu.’
12. Mimi ni nyumba ya majoka na nge, mimi ni nyumba ya udhalili. Dunia hii ni ya kupita (ni mpito), akhera ni ya kudumu milele, kwa hivyo niimarishe na usinibomoe. Ee mwanaadam! Tenda mema kwanza badaye ndiyo uje kwangu, hapo tu ndipo utakuwa na raha na utaishi bila dhiki.

## **SURA YA 6**

### **USAFISHE MOYO WAKO DHIDI YA KUIPENDA DUNIA**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Enyi Wanaadam! Mimi Sikuwaumba nyinyi ili kujiogezea nguvu kutokana na upungufu wenu, na wala si kwa ajili ya kujifurahisha na upweke, si kwa ajili ya kujinufaisha wala kujikinga kutokana na madhara, lakini Mimi nimewaumba ili mniabudu daima na kunishukuru kwa wingi na kunihimidi usiku na mchana..

## **Hadithi Qudsi**

2. Lau kama wa mwanzo wenu na mwisho wenu, walio hai kati yenu na waliofariki mionganoni mwenu, mdogo na mkubwa wenu, watu huru na watumwa, nyinyi nyote mkiungana na majini kunitii Mimi msingeniongezea chochote katika ufalme wangu japo uzani wa wa punje dogo kabisa. Lau kama wa mwanzo wenu au wa mwisho wenu walio hai kati yenu na waliofariki mionganoni mwenu, mdogo wenu au mkubwa wenu, watu huru au watumwa, nyinyi nyote mkiungana na majini kuniasi, hamtaweza kupunguza uzani mdogo kabisa katika ufalme wangu.

Hakika mwenye kufanya jitihada basi ni kwa ajili ya nafsi yake kwani Mwenye Enzi Mungu Anajitosheleza kutokana na walimwengu.

### **VITENDO VYEMA VITANO VITANG'ARISHA KABURI LAKO**

#### **ALLAH (S.W. T.) ANASEMA:**

1. Ee mtumwa wa dinar na dirham. Mimi (Allah) sikuumba hizo sarafu ila kwa ajili yenu mijipatie mahitaji yenu kama chakula, mavazi na mtoe sadaka kama nilivyoamrisha.
2. Mmechukua kitabu changu na kukiweka chini ya miguu yenu na kuchukua dunia na kuiweka juu ya vichwa vyenu.

Mmetukuza nyumba yenu; lakini mmedharau nyumba zangu.

3. Mmetukuza nyumba zenu na kufarijika kwa kuishi humo; lakini hampati raghba na hamu ya kuja kwangu. Basi nyinyi sio watumwa wema walio huru.

## **Hadithi Qudsi**

4. Ee mtumwa wa dunia! Kwa hakika mfano wenu ni kama kaburi lilopambwa kwa marumaru, kwa nje linapendeza lakini ndani kwake kubaya.
5. Ee mwanaadangu! Taa iliyowashwa juu ya paa la nyumba mwanga wake hauna manufaa yoyote kwa kiza kilichopo ndani ya nyumba, ni hivyo vivyo maneno yenu mazuri hayana manufaa ikiwa vitendo vyenu ni viovu.
6. Ee Mwanaadam! Takasa vitendo vyako na usiombe; kwa sababu Mimi nitakujalia zaidi kuliko wale wanaoomba.

## **SURA YA 7**

### **BINADAMU AMEUMBWA KWA AJILI YA LENGO ADHIM**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Ee mwanaadangu! Mimi (Allah) Sikuwaumba bila lengo maalum au kuwaumba nyinyi bure.
2. Mimi (Allah) usifikiri sijui vitendo vyenu.
3. Kwa hakika nyinyi hamtapata ninayomiliki Mimi; isipokuwa kwa subira juu ya mambo msiyoyapenda yanayowakabili wakati wa kutafuta Ridha Yangu.
4. Subra katika utii wangu ni rahisi kuliko uvumilivu wa moto wa Jahannam.

## **Hadithi Qudsi**

- 5) Adhabu duniani ni nyepesi zaidi kuliko ya kale (Akhera).
- 6) Ee Mwanaadam! Nyote mmepeotea ila yule Niliyemuongoza.
7. Nyote ni wagonjwa ila yule Niliyemponya..
8. Nyote ni wenyе dhambi ila yule Nileyemkinga.
9. Nyote ni maskini ila yule Niliyemtajirisha.
10. Nyote mtaangamia ila yule Niliyemnusuru.
11. Kwa hivyo ombeni msamaha Kwangu (Allah) ili Mimi niwaonee huruma.
12. Msijaribu kuficha dhambi (maovu yenu) kwa yule ambaye dhambi zenu kwake zinajulikana

## **SURA YA 8**

**WANAADAM! KWA SABABU GANI NYINYI HAMZILINDI  
NAFSI ZENU DHIDHI YA GHADHABU YA MUNGU WENU?**

**ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Ee mwanaadanu! Msiwalani viumbe wangu, kwa sababu lana isije ikarudi kwenu. Ee Mwanaadam! Angalia mbingu zangu zimening'inia angani bila nguzo kutokana na jina moja mionganii mwa Majina Yangu.
2. Miyo yenu haitapata uongofu ila kwa nasaha kutoka kwenye kitabu changu.

## **Hadithi Qudsi**

3. Ee Nyinyi! Watu! Kama lilivyo jiwe haliyayuki majini; vivyo hivyo mawaidha hayanufaishi mioyo migumu.
4. Ee Wanaadam! Kwa sababu gani hamujiepushi na haramu, na huendelea kufanya dhambi wala hamuogopi Moto?
5. Kwa sababu gani hamujilindi dhidhi ya ghadhabu yangu, Rahmani?
6. Kama isingekuwa kwa ajili ya rukuu za wazee, watoto wachanga wanaonyonya, wanyama wanaotafuta malisho, vijana wenyenyekevu, Mimi Ningelifanya mbingu kuwa chuma. Ardhi kuwa shaba, na udongo kuwa changarawe. Wala Nisingeruhusu hata tone moja la mvua kunyesha kutoka mbinguni na kuota (mmea) hata chembe moja juu ya ardhi. Mimi ningewateremshia adhabu mbaya mno.

## **SURA YA 9**

### **HAKUNA MMOJA ALIYEKUWA MBORA KULIKO MWENZI**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

Ewe Mwanaadam! Bila shaka ukweli umewajia kutoka kwa Mola wenu.

1. Yeyote anayetaka kuamini, basi na aamini, na yeyote asiyetaka kuamini basi na asiamini.
2. Kwa hakika nyinyi hamfanyi wema ila kwa yule aliyewafanya

## **Hadithi Qudsi**

wema.

3. Nyinyi hamuwi na huruma (mapenzi) na jamaa zenu mpaka wao wawe na huruma na nyinyi.
4. Wala hamzungumzi ila na yule anayezungumza na nyinyi.
5. Nyinyi hamumlishi chakula ye yote ila kwa aliywalisha.
6. Wala hamumfanyii uadilifu ila yule aliyekufanyieni uadilifu.
7. Nyinyi hamumuaheshimu ila yule aliywaheshimu.
8. Hakuna ye yote mbora kwa mwingine: Kwa hakika Waumini ni:
  - i) Wale wanaoamini Mungu (Allah) na wajumbe Wake aliowatuma na wanawafanyia wema wale waliowakosea.
  - ii) Huwa wema kwa wale waliokuwa waovu kwao.
  - iii) Huwa na huruma juu ya wale ambao wamevunja uhusiano wa ujamaa.
  - iv) Huwapa wale wanaowanyima.
  - v) Waadilifu kwa wale waliowafanyia hiana.
  - vi) Huzungumza na wale ambao wanaojitenga kuzungumza nao.
  - vii) Kuwa na heshima na wale wasiowaheshimu.

## **Hadithi Qudsi**

### **SURA YA 10**

**KWA HAKIKA BINADAMU AMEIDHULUMU**

**NAFSI YAKE:**

**ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Enyi watu! Hii dunia ni makazi (nyumba) ya yule mtu asiye na makazi (nyumba). Mali hii ya dunia ni kwa ajili ya yule mtu asiye na mali .Na kwa hivyo asiye na uhakika wa kesho (kuamini Akhera) hujikusanya mali hapa duniani. Yule asiye na imani na maarifa juu ya Allah (s.w.t.) hutamani hii dunia.
2. Kwa hivyo yule anajiyeipatia zawadi (mali) nyingi mno katika dunia hii ya muda mfupi (mpito) na kufuata (endekeza) matamanio yake basi bila shaka anadhulumu nafsi yake. Yeye ni mwenye hatia (dhambi) mbele ya Allah (s.w.t.) na kusahau (ghaflika na) Akhera. Uhai wake (maisha ya dunia) umemhadaa.

### **SURA YA 11**

**YULE ANAYEMDHALILISHA MWENYE IMANI**

**ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

Enyi Wanaadam! Kumbukeni neema zangu nilizowapeni. Kama ambavyo hamwezi kuongoka katika njia ila kwa dalili; kadhalika bila elimu hamwezi kupata njia ya kuenda peponi. Na kama

## Hadithi Qudsi

---

ambavyo hamwezi kukusanya mali bila juhud, vivyo hivyo hamwezi kuingia Peponi bila ya subra na ibada, basi jikaribisheni kwangu kwa Swala za Sunna, tafuteni radhi zangu kwa kuwafurahisha maskini. Kwa hakika ridhaa Yangu haiachani nao hata kidogo, pendeleeni kukaa na maulamaa kwani rehma haiachani nao abadan.

Ewe Musa! Nisikilize ninachosema ni kweli tupu bila shaka. Kwa hakika yule anayemfanyia kiburi maskini basi Mimi siku ya Kiyama Nitamfufua kama chembechembe iliyokuwa chini ya miguu ya watu.

Yeyote anayemdhalilisha mwislamu Mimi (Allah) nitamdhilisha mara sabini.

Yeyote atayemnyenyeka mwanachuoni na wazazi wake, Mimi nita-mtukiza hapa duniani na kesho Akhera.

Yeyote anayemfedhehesha mwislamu na muumini kwa sababu ya ufukara wake basi huyo anapambana na Mimi.

Yeyote anayempenda muumini kwa sababu Yangu, Malaika watao-nana naye hapa duniani (kisiri) na kesho Akhera dhahiri.

## **Hadithi Qudsi**

### **SURA YA 12**

**KILA KITU KITAANGAMIAILA MWENYEZI MUNGU**

**ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Enyi wanaadam! Nitiini Mimi kadri ya mahitaji yenu kwangu. Na mnikhali kama mtaweza kuvumilia moto wa Jahannam. Kusanyeni mali duniani kufuatana na muda wa uhai wenu. Pata wekevu wa Akhera kufuatana na muda wa kuishi huko (Akhera), Msifikiri vifo vyenu viro mbali na nyinyi. Kujaliwa zawadi kusi-wafanye mfikiri dhambi zenu zimefichika.
2. Kila kitu kitaangamia ila Mimi. Laiti mngeuogopa moto wa Jahannam kama mnavyoogopa umaskini, bila shaka Mimi ningewafanya huru kwa kuwatosheleza kwa utajiri bila nyinyi kutarajia.
3. Laiti mngekuwa na shauku ya Pepo kama mlivyo na shauku na dunia, Ningewajaalia raha kote kote, (duniani na akhera). Msizifishe nyoyo zenu kwa kupenda dunia kwani na punde tu itaondoka.

## **Hadithi Qudsi**

### **SURA YA 13**

**JIENDELEZE KWA AJILI YANGU (ALLAH)**

**NA JIFURAHISHE KWA NEEMA ZANGU**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Enyi Wanaadam! Mishumaa mingapi imezimwa na upepo? Wafanya ibada wangapi ibada zao zimeharibika kutokana na kiburi? Mafukara wangapi umasikini wao umewaharibu? Matajiri wangapi utajiri wao umewaharibu? Watu wangapi wenyе afya njema afya zao zimewaharibu? Wanavyuoni wangapi elimu zao zimewaharibu?

Enyi Wanaadam! Limeni kwa ajili Yangu ili mfaidike kutoka Kwangu. Mniombe Mimi na nitumikieni. Kwa hakika manufaa yenu yote hutoka Kwangu, ambayo hakuna jicho limewahi kuona, sikio lolote kusikia wala moyo wa mwanaadamu kuwaza. Hazina Yangu haitamalizika kamwe. Hakuna upungufu katika ufalme Wangu. Mimi ni Mpaji, Mkarimu Mno.

Ewe Mwanaadam! Dini yako ni nyama na damu yako. Dini yako ikitengemaa basi nyama na damu yako itatengemaa. Dini yako iki-haribika basi nyama yako na damu yako itaharibika.

Usiwe kama mshumaa unaowapa mwangaza watu lakini hujiunguza wenyewe. Ondoа mapenzi ya dunia moyoni mwako. Kwa hakika Mimi sichanganyi mapenzi Yangu na mapenzi ya dunia katika moyo

## Hadithi Qudsi

mmoja huo huo; kama maji na moto visivyoweza kukusanyika pamoja katika chombo kimoja: kwa hivyo iherumie nafsi yako kwa kutafuta riziki.

Kwa hakika riziki zenu ni za kugawiwa. Mwenye pupa hunyimwa. Bakhili ni mwenye kulaumiwa. Neema hazidumu na mauti yamepangwa. Hekima bora ni kumwogopa Mwenyezi Mungu. Utajiri uliyo bora kabisa ni kutosheka; na akiba bora kuliko zote ni ucha Mungu.' Ubaya wa wema wenu ni uongo; uovu wa nasaha zenu ni usengenyaji. Na wala Mola wako si Mwenye kuwadhulumu waja.

## SURA YA 14

### UISLAM ULIO HAI

**ALLAH (S.W.T.) ANASEMA: “ENYI MLIOAMINI! KWA NINI MNAZUNGUMZIA MAMBO MSIYO YAFANYA?”  
(QUR’AN 61:2)**

Kwa sababu gani mnawakataza watu kutenda maovu ilihali wakati huo huo hamkatazi nafsi zenu (kujizuia nafsi) kutenda hayo maovu?

Kwa sababu gani mnaamrisha kutenda mambo ambayo nyinyi wenyewe hamyatendi?

Je unao uwezo mikononi mwako wa kujikinga na moto wa Jahannam?

Kwa sababu gani mnakusanya vitu ambavyo hamvili?

Kwa sababu gani mnachelewesha kuomba toba (msamaha) siku bada ya siku; na mnangoja mwaka hadi mwaka? Je! Mmejipatia

## Hadithi Qudsi

kinga dhidhi ya kifo?

Je mna uhakika wa kuingia Peponi?

Je hizo neema zimewapatia muda wa nyongeza?

Je mmejipatia kiburi kutokana na Allah (s.w.t.) kutimiza matumaini yenu yasiyo na kikomo?

Kwa hivyo msipate kiburi kutokana na afya zenu njema na usalama

Siri zenu zimefichuka na mapazia yameondoshwa.

Kwa hivyo Muogopeni Allah (s.w.t.) enyi watu wenyewe hekima.

Kuweni waangalifu (kutokana na faradhi zenu) kwa Allah (s.w.t.).

Inafaa mjitangulizie na ya mustakabali kwa kutumia uwezo mliokuwa nao sasa mikononi mwenu.

Ee Mwanaadam! Tafakari juu ya kitendo unachotaka kutenda. Kwa hakika wewe uko katika kutelekeza maisha yako.

Tokea ulipotoka tumboni mwa mama yako (kuzaliwa duniani) unakaribia kaburi lako.

Kwa hivyo usiwe kama kuni inayojiunguza kwa ajili ya wengine.

Bila Shaka! Kwa hakika! Hakuna mungu ila Allah (s.w.t.), Muhammad (s.a.w.) ni kiumbe na Mjumbe Wangu (Allah)

## Hadithi Qudsi

### SURA YA 15

#### NITII MIMI ILI UWEZE KUWA NA UWEZO KAMA MIMI ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:

1. Ee mwanaadamu, Mimi nipo hai milele. Mimi kamwe sitakufa.
2. Tenda kama nilivyokuamrisha.
3. Jilinde na niyokukataza; ili Mimi nikuaalie uhai wa milele (Akhera).
4. Ee mwanaadam! Mimi ni Mfalme ambaye ufalme Wake kamwe hautapotea.
5. Mimi ninaposema “Kuwa” Basi “Huwa” papo hapo.
6. Tii amri zangu na epukana na makatazo yangu, ili ukisema kitu ‘Kiwe’ basi ‘Kiwe.’
7. Ikiwa maneno yako ni matamu lakini vitendo vyako ni viovu basi wewe ni kiongozi wa wanafiki.
8. Ikiwa wajih (uso) ni wa kupendeza lakini undani wako ni mbaya basi wewe ni wa kuangamia zaidi kuliko wale walioangamizwa.
9. Ee mwanaadanu! Hakuna mmoja wenu ataingia Peponi ila:
  - a) Yule ambaye amekuwa mnyenyeketu mbele ya utukufu wa Allah (s.w.t.).
  - b) Yule aliyejihini nafsi yake dhidhi ya Matamanio kwa ajili Yangu na kuitisha wakati wake kwa kunikumbuka Mimi (Allah s.w.t.).

## **Hadithi Qudsi**

- c) Yule aliyetumia uhai wake kunikumbuka Mimi (Allah.s.w.t.).
- d) Yule anayewaonea huruma wageni.
- e) Yule anayewasaidia maskini.
- f) Yule anayewahurumia walioathirika na misiba.
- g) Yule anayewakirimu mayatima na anakuwa kama baba mwenye huruma na kuwahurumia wajane, anakuwa kama mume mwenye huruma kwao.
- h) Yule mwenye sifa hizi, akinita Mimi nitamjibu mara moja na anaponiomba Nitampatia.

## **SURA YA 16**

**MPAKA LINI WEWE BINADAMU UTATENGANA**

**NA MIMI (ALLAH S.W. T.)**

**ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Ee Wanaadam! Mpaka lini mtanisahau Mimi?
2. Mpaka lini nyinyi mtakanusha kuwepo kwangu (mtanikataa Mimi)?
3. Hadi lini mtakufuru neema zangu na riziki yenu kila siku hutoka Kwangu.

## **Hadithi Qudsi**

4. Hadi lini mtakanusha Mimi kuwa Mola wenu na wala hamna Mola mwingine ila Mimi.
5. Hadi lini mtaendelea kutonijali? Wakati Mimi huwajali nyinyi?
6. Nyinyi hamuna Mungu mwingine ila Mimi.
7. Kwa muda gani mtaendelea kutonijali Mimi? Mimi kamwe siku-tendei dhulma,
8. Mkiwa wagonjwa hutafuta dawa kwa ajili ya miili yenu kwa daktari; lakini nani atawasamehe dhambi zenu?
9. Bila shaka hulalamika kutokana na uamuzi Wangu.
10. Ikiwa mmoja wenu hakupata chakula kwa siku tatu tu anasema: ‘Mimi ni mwovu na sina kheri.’ Kwa hakika huyo amekufuru fadhila zangu.
11. Na yule asiyetua Zaka kutoka kwenye mali yake kwa hakika amedharau kitabu changu.
12. Na anayejua kuwa wakati wa Swala umewadia na asisali, kwa hakika kaghafilika na Mimi.

## **Hadithi Qudsi**

### **SURA YA 17**

**NIITE, NAMI NITAKUITIKIA**

**ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

Ee mwanaadunu! Kuwa na subra na mnyenyekevu. Mimi nitakuinua.

Nishukuru Mimi; na Mimi nitakuzidishia..

Tafuta msamaha kwangu na Mimi nitakusamehe.

Niite Mimi; na Mimi nitakuitika.

Niombe Mimi; na Mimi nitakupa.

Toa sadaka kama nilivyokuamrisha na Mimi nitakubariki kwa ukarimu Wangu.

Kuwa na huruma (mapenzi) na jamaa yako na mimi nitakujalia umri mrefu.

Ombo afya njema wakati unayo afya njema ili kurefusha siha.

Uombe usalama katika upweke.

Ombo kwa moyo safi (unyoofu) kwa ajili ya utakatifu.

Ombo Ucha-Mungu kwa kutubia maovu.

Jipatie nasaha kwa kufanya ibada Yangu kwa maarifa..

## **Hadithi Qudsi**

Jipatie uhuru kutokana na kutosheka.

Ee mwanaadangu! Vipi utatamani umuhimu wa ibada wakati umeshi-ba?

Vipi utautia nuru moyo wako wakati unalala sana?

Vipi utamogopa Allah (s.w.t.) wakati unaogopa umaskini?

Vipi! Utapata ridhaa ya Allah (s.w.t.) kwa kuwdhalilisha maskini na mafukara?

## **SURA YA 18**

### **HAKUNA HEKIMA BILA KUTAFAKARI**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Enyi watu! Hakuna hekima kama kutenda kwa kutafakari.
2. Wala hakuna uchamungu kama kujizuia kuwaudhi wengine.
3. Hakuna nasaba bora zaidi kuliko adabu.
4. Hakuna uombezi bora kuliko toba.
5. Hakuna ibada kama ilimu na hakuna Swala ila iwe na unyenyekevu na khofu ya Allah (s.w.t.).
6. Hakuna ufukara bora ila uwe na subira.
7. Hakuna ibada kama kuwafikiwa.

## **Hadithi Qudsi**

8. Hakuna rafiki mzuri kama akili; na hakuna rafiki mbaya zaidi kuliko ujinga.
9. Ee mwanaadanu! Jishughulisse na ibada Yangu, nitaujaza moyo wako utajiri, mikono yako ukarimu, na mwili wako raha.
10. Usisahau utajo wangu. La sivyo nitaujaza moyo wako ufukara, mwili wako tabu, kifua chako matatizo na shida, nitaujaza mwili wako maradhi na wewe kuiona dunia ngumu.

## **SURA YA 19**

### **KWA HAKIKA KIFO KITAFICHUA VITENDO VYAKO**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Ee mwanaadam! Kifo kitafichua siri zako.
2. Siku ya hukumu itakuwa mtihani wa vitendo vyako.
3. Kitabu cha vitendo vyako kitafichua vitendo vyako,
4. Unapotenda dhambi usiangalie udogo wa hilo dhambi; lakini fikiria nani unamuasi?
5. Ikiwa unapata riziki hata kidogo usifikirie udogo wake, lakini fikiria nani anakuruzuku
6. Ee mwanaadanu! Usifikirie umesalimika kwa ghadhabu Yangu! Kwa sababu ghadhabu Yangu imefichika kama harakati za mchwa katika usiku wa kiza totoro.

## **Hadithi Qudsi**

7. Ee Wanaadamu! Mmetekeleza faradhi kama nilivyowaagiza?
8. Je! Mmewahurumia maskini na mafukara kwa nafsi zenu na mali zenu?
9. Je! Mmekuwa wema kwa wale waliokuwa waovu kwako?
10. Je! Mmewasamehe wale waliowatendea dhulma?
- 11.) Je! Mmekuwa na uhusiano mwema na wale jamaa ambaao wamekata uhusiano na nyinyi?
12. Je! Mmekuwa waadilifu kwa wale waliowasaliti?
13. Je! Mnazungumza na wale waliowatenga?
14. Je! Mmewafunza wanenu tabia njema?
15. Je! Mmewauliza wanavyuoni wenu kuhusu maisha yenu ya hapa duniani na kesho (Akhera)?
16. Kwa Hakika Mimi siangalii sura zenu wala miili yenu, lakini Ninangalia nyoyo zenu na vitendo vyenu. Mimi huridhika na mambo hayo.

## **Hadithi Qudsi**

### **SURA 20**

#### **BILA SHAKA WAKATI WA KUTOA HESABU UKO KARIBU**

**ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Ee mwanaadanu! Angalia nafsi yako na viumbe wangu.
2. Ukimuona hata mmoja mwenye utukufu zaidi yako basi mheshimu, vinginevyo heshimu nafsi yako kwa kutubia na kuten-da vitendo vyema. Ikiwa unaheshimu nafsi yako.
3. Enyi! Waumini! Kumbukeni fadhila za Allah (s.w.t.) alizowajalia.
4. Muogopeni Allah kabla siku ya hukumu-Tukio Adhimu (Angali Sura-Ya-Waqia). Hiyo ni siku ya msiba mkuu: Muda wake utakuwa ni miaka elfu hamsini; siku hiyo ambayo hakuna mtu atawenza kusema wala kutoa udhuru. Siku ya balaa kuu. Siku ya parapanda. Ni Siku ya kuhuzunisha. Siku hiyo ambayo hakuna nafsi itakuwa na udhibiti juu ya nafsi ya mwingine. Siku ambayo itakuwa ya maangamizi. Siku ya mtikisiko wa ardhi. Siku ya balaa ya kutisha (zilzal). Kwa hivyo muogopeni Allah (s.w.t.) kwa ajili ya Siku ambayo milima itaangamia kutohana na mtetemeko wa ardhi.

Siku hiyo ya kutisha hugeuza watoto (vijana) kuonekana wazee. Msiwe kama wale waliosema tumesikia na tumeasi.

## Hadithi Qudsi

### SURA YA 21

#### KUANGAMIA KWAKO HUTOKANA NA ULIMI WAKO

##### ALLAH (S.W.T.) ASEMA:

1. Ee Nyinyi Mlioamini! Mkumbukeni Allah (s.w.t.) daima na kwa wingi.
2. Ee Musa mwana wa Imran! Mtaalam wa kueleza, sikiliza maneno Yangu: Kwa hakika ! Mimi ni Mfalme. Bwana anayetoa zawadi.
3. Hakuna haja ya mkalimani baina yako na Yangu.
4. Muonye yule anayepokea riba na yule anayewaasi wazazi wake kuhusu ghadhabu ya Rahman na miale ya moto wa Jahannam.
5. Ee mwanaadanu! Ukiona moyo wako umekuwa mgumu, mwili wako umeathirika na magonjwa na hupati riziki, basi uelewe kwamba umenena maneno yasiyokuletea faida.
6. Ee mwanaadam! Dini yako haitatengemaa mpaka wewe utakapotengemaa ulimi wako.
7. Na moyo wako hautatengemaa mpaka utapotengemaa ulimi wako.
8. Na ulimi wako hautatengemaa mpaka umnyenyeknee Mola wako.
9. Unapotafuta makosa ya watu wengine bila kutafuta makosa kati-ka nafsi yako basi umemfurahisha shetani na kumkasirisha Mungu wako.
- 10 Ewe Mwanadamu! Ikiwa ulimi wako ni mkali kama simba na

## **Hadithi Qudsi**

ukiacha bila kudhibiti, basi huo ulimi utakuangamiza. Maangamizi yako yatasababishwa na ulimi wako ambayo yapo katika ncha ya ulimi wako.

## **SURA YA 22**

### **NA MIMI NI BWANA MUNGU WAKO WEWE UNITAMBUE**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

Enyi wanaadam! Kwa hakika shetani ni adui wenu dhahiri, basi mfanyeni kuwa adui wenu.

Tendeni vitendo vyema kwa ajili ya siku ambayo nitawakutanisha mbele Yangu (Allah s.w.t.) kwa makundi kwa makundi.

Mbele ya Mungu mtasimamishwa katika safu na mtasoma vitabu vya vitendo vyenu neno kwa neno. Nyinyi mtaulizwa mliyoyafanya kwa siri na kwa dhahiri.

Kisha wacha-Mungu wataelekea Peponi makundi kwa makundi; na wenye dhambi watapelekwa Jahannam makundi kwa makundi.

Huwatosheni miadi na kiaga kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Umezungumza yasiyokuhusu.

Dini yako haitanyooka mpaka unyooke ulimi wako na moyo wako, hautanyooka moyo wako mpaka unyooke ulimi wako, na hautanyooka mpaka umuonee haya Mola wako. Na unapoangalia aibu za wengine na ukasahau zako, basi umemridhia shetani na kumuudhi

## **Hadithi Qudsi**

Mola.

Eee mwanaadamu! Ulimi wako ni simba, ukiuacha utakuangamiza, na kuangamia kwako kuko katika ncha ya ulimi wako.

- i) Na Mimi ni Allah, nitambueni.
- ii) Mimi ni Mpaji kwa hivyo nishukuruni.
- iii) Mimi ni Msamehevu, kwa hivyo ombeni msamaha kutoka Kwangu.
- iv) Mimi ni Mtegemewa kwa hivyo nitegemeeni.
- v) Mimi ni Mjuaji wa siri, hivyo niogopeni.

## **SURA YA 23**

### **BISHARA NJEMA ZILIZOTANGAZWA KWA AJILI YA WATU WATAKAOENDA PEPONI**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Allah (s.w.t.) Anashuhudia kwamba hakuna Mungu ila Yeye. Pia malaika wenye elimu wenye kusimamia uadilifu wanatoa ushahidi kwamba hakuna Mungu ila Yeye, Mtukufu, Mwenye Hekima, na Mwadilifu. Hakuna ye yeyote mwingine ila Yeye (Allah s.w.t) Mwenye Enzi na Mwenye Hekima.
2. Kwa hakika dini iliyo kweli na kukubalika mbele ya Allah ni Uislam tu. (Quran 3:10).

## **Hadithi Qudsi**

3. Wabashirie watu wema Pepo, na kila mwasi atahili na kupata hasara.
4. Yule anayemjua Allah (s.w.t.) na kutii amri zake ataokoka.
5. Yule anayemtambua shetani na kutomtii, amesalimika
6. Mtu anayejua haki na kuifuata, amesalimika. Anayeyitambua batili na kujiepusha amefaulu.
7. Yule anayetambua dunia (ya kuhiliki) na kutoijali hiyo dunia ameitakasa nafsi yake.
8. Yule anayearmini kuwepo kwa Akhera (maisha bada ya kifo) na kuitafuta, basi ameipata.
9. Kwa hakika Mwenyezi Mungu (Allah s.w.t.) humongoza yejote amtakaye, na nyote mtarejeshwa kwake ambaye ni hitimisho kwa binadam.
10. Ee mwanaadangu! Ikiwa Mwenyezi Mungu (Allah s.w.t.) Amechukua dhamana kuwapa riziki basi bidii zote za kutafuta riziki ni za nini?.
11. Na ikiwa unaamini hao viumbe wote ni Wangu, basi kwa sababu gani kufanya ubakhili?
12. Na ikiwa wewe unaamini Iblisi (shetani) ni adui Wangu, basi kwa sababu gani unaghafilika?
13. Ikiwa Siku ya hukumu na kupita juu ya *Sirat* (Daraja ya kuvuka kuendea Peponi) ni kweli, basi kwa sababu gani unakusanya mali? Ikiwa adhabu ya Allah ni kweli kwa nini unaasi?

## **Hadithi Qudsi**

14. Na ikiwa unaamini kwa uyakinifu kuwa zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu ni Pepo; kwa sababu gani unakuwa mlegevu kuitafuta?
15. Ikiwa kila kitu kiko kwenye qadhaa na qadar yangu kwa nini ubabaike?
16. Kwa hivyo usikate tamaa, na ikiwa unapenda dunia basi usifurahikie mno faida ya dunia.

Ili msihuzunike na yale yaliowapata wala msifurahie kwa yale niliyowapa.

## **SURA YA 24**

### **UWE KWA AJILI YANGU NA MIMI NITAKUWA KWA AJILI YAKO**

**ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Jikusanyie akiba kwa ajili ya akhera kwa kutenda mema kadiri ya uwezo wako. Kwa hakika safari ni ndefu mno. Kwa hivyo liimarishe jahazi lako. Hakika bahari ina kina kirefu, na punguza mzigo (dhambi) kwani njia ni nyembamba mno.
2. Takasa vitendo vyako; kwa hakika Mkaguzi (Allah s.w.t.) ni Makini huona kila kitu.
3. Akhirisha usingizi wako hadi kaburini, fahari yako iko kwenye mizani. Matamanio yako ni Pepo na raha yako iko akhera. Shauku yako ni Hurul'ain.

## **Hadithi Qudsi**

4. Punguza anasa zako mpaka uingie Peponi.
5. Akhirisha mapumziko yako mpaka Akhera (Jibidishe daima) ili upate Pepo.
6. Kuwa Kwa ajili Yangu na Mimi nitakuwa kwa ajili yako.
7. Tafuta ukaribu Kwangu kwa kutengana na hii dunia.
8. Jiepushe na moto wa Jahannam kwa kuwachukia waovu na kuwapenda wacha-Mungu.
9. Kwa hakika Allah (s.w.t.) Hatapoteza malipo ya watu wema.

## **SURA YA 25**

### **JILINDE NA JIHURUMIE NAFSI YAKO DHIDI YA MOTO WA JAHANNAM**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANA SEMA:**

1. Enyi wanaadunu! Vipi mnadiriki kuniasi Mimi, wakati hamuwezi kuvumilia joto la jua na joto la jangwani? Kwa hakika katika Jahannam kuna tabaka saba za moto na humo kuna moto baadhi unaounguza baadhi yake.
2. Katika kila tabaka ya Jahannam kuna mabonde elfu sabini ya moto.
3. Katika kila bonde kuna sehemu elfu sabini za moto.

## Hadithi Qudsi

---

4. Katika kila sehemu kuna miji elfu sabini ya moto.
5. Katika kila mji kuna ngome elfu sabini za moto.
6. Katika kila ngome kuna nyumba elfu sabini za moto.
7. Katika kila nyumba kuna vyumba elfu sabini nya moto.
8. Katika kila chumba kuna visima elfu sabini nya moto.
9. Katika kila kisima kuna kasha elfu sabini za moto.
10. Katika kila kasha kuna miti elfu sabini ya Zaqqum.
11. Chini ya kila mti wa Zaqqum kuna vizingi elfu sabini nya moto, na kila kigingi kuna minyororo elfu sabini ya moto. Katika kila minyororo kuna nyoka elfu sabini wa moto.

Urefu wa kila nyoka ni dhiraa elfu sabini. Katika kila tumbo ya nyoka kuna rundo kubwa (kama bahari) la sumu nyeusi ambamo kuna nge elfu sabini wa moto. Kila n'ge huwa na mikia sabini ya moto. Urefu wa kila mkia huwa mara elfu sabini ya mkato wa uti wa mgongo. Kila mkato una uzito wa ratili elfu sabini (kila ratili ni gram 450) ya sumu yenyе rangi nyekundu.

Mimi (Allah s.w.t.) Ninaapa kwa nafsi Yangu, Mlima wa Sinai, Kwa Kitabu kilichoandikwa, Kwa Kitambaa kilichofunikwa juu ya Al-Kaaba, Baitul Ma'amur na kwa paa lilonyanyuliwa na kwa bahari iliyofurika.

Ee mwanaadanu! Mimi sikuumba moto huu na hii Jahannam ila ni kwa ajili ya Makafiri, mabakhili, wambeya, wale waliokosa radhi za wazazi wao, wazinifu, wala riba, wakusanyaji mali ya haramu, wanaosahau Kurani na kutojali majirani. Ila wale tu watakaoomba

## **Hadithi Qudsi**

toba na kurekebisha maisha yao kwa kutenda vitendo vyema.

Ee Waja wangu! Mjihurumie nafsi zenu. Kwa hakika miili yenu ni dhaifu sana (isiyo na nguvu). Safari ni ndefu mno, Mzigo (wa dhambii) mzito mno, Njia ipo nyembamba na Moto umewaka sana. Atayeita watu ni Israfil (Mmoja katika Malaika wakuu)! Hakimu ni Bwana (Mmiliki) wa walimwengu wote

## **SURA YA 26**

### **ZAWADI YA MILELE KWA AJILI YA WATENDA MEMA**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Enyi watu! Vipi mnaweza kufurahishwa na kuendekeza hii dunia ya kumalizika, neema zake ni zenyе kupita tu, maisha yake ni yenye kukatika. Uhai wa mtu hapa duniani huwa mfupi mno.
2. Kwa hakika kwangu kuna pepo kwa ajili ya wanaonitii yenye milamgo minane.
3. Katika kila Pepo kuna bustani elfu sabini za Zafrani na katika kila bustani kuna miji elfu sabini ya Lulu na Marjan.
4. Katika kila jiji kuna kasri elfu sabini za Yakut.
5. Katika kila kasri kuna vyumba elfu sabini vya dhahabu.
6. Katika kila chumba kuna majukwaa elfu sabini ya fedha.

## **Hadithi Qudsi**

---

7. Juu ya kila jukwaa kuna meza elfu sabini.
8. Juu ya kila meza kuna sahani elfu sabini za johari.
9. Ndani ya kila sahani kuna aina ya vyakula elfu sabini.
10. Na kila jukwaa limezungukwa na viti vya kifalme elfu sabini vilivytengenezwa kwa hariri na hariri za taraza.
11. Na kila kitanda kimezungukwa na mito elfu sabini yenyе maji ya uhai, maziwa, kileo na asali safi.
12. Katika kila mto kuna matunda aina elfu sabini.
13. Kadhalika katika kila chumba kuna mahema elfu sabini ya rangi ya zambarau.
14. Katika kila hema kuna matandiko elfu sabini.
15. Juu ya kila tandiko kuna Huur (wanawake maalum wa Peponi) wenyе macho makubwa makubwa.
16. Na kila tandiko kuna Hurul-ayn elfu sabini, mikononi mwao kuna mapambo aina elfu sabini kana kwamba mayai yaliyohi-fadhiwa kwa uangalifu.
17. Juu ya kila kasri kuna kuba elfu sabini za kafur.
18. Katika kila kuba kuna zawadi elfu sabini kutoka kwa Rahman (Allah s.w.t.), ambazo hazikuonwa na jicho, sikio halijawahi kusikia wala mioyo ya wanadamu haijawahi kuwaza.
19. Patakuwa na matunda ya kila aina yanayopendwa.

## **Hadithi Qudsi**

20. Kutakuwa na nyama za ndege wa kila aina zinazopendwa kuli-wa.
21. Kutakuwa na Huurl-‘ayni wanaong’aa mifano ya lulu zilizohifadhiwa.
22. Ni malipo kwa ajili ya wale waliotenda mema (Kurani Tukufu: 56:23-24).

Hakutakuwa na kifo, majonzi, masikitiko au kudhoofika. Hakutakuwa na ibada: Swala ya aina yoyote, Saumu, ugonjwa, kushikwa na haja kubwa wala ndogo, Hakutakuwa kamwe na tishio, uoga wa aina yoyote na hakuna atayewatoa humo na wala hawatahisi uchovu.

Kwa hivyo yejote anayetafuta ridhaa Yangu, (Allah) nyumba ya utukufu na ujirani Wangu (ukaribu na Mimi), basi huyo mtu atafute kwa kutoa sadaka, kutengana na dunia na kutosheka na kidogo alichojaaliwa.

## Hadithi Qudsi

---

Mimi Allah (s.w.t.) nashuhudia kwa nafsi Yangu (Allah) kwamba Nabii Isa (a.s.) na Nabii Uzair (a.s.) wanaofikiriwa kuwa ni wanangu (Wana wa Mungu) na Wakristo na Mayahudi; hao ni viumbe wangu wawili katika manabii Wangu niliowatuma kwa binadamu.

## SURA YA 27

### **KUWA MNYENYEKEVU ILI UNIJUE MIMI (ALLAH S.W.T.). UJIPATIE MAARIFA JUU YANGU**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Ee mwanaadam! Mali) yote ni yangu na wewe kiumbe ni mtumwa Wangu.
2. Hakuna chohote kilichokuwa chako; isipokuwa ulichokula na unachovaa na vyote kumalizika.
3. Chochote ulichotoa kama sadaka hugeuka cha milele. Chochote unachokusanya (hodhi) hakikuletei faida ila huchuma chuki.
4. Kwa hakika wewe binadamu umegawanyika katika sehemu tatu: Sehemu moja ni kwa ajili Yangu na sehemu moja nyingine ni kwa ajili yako na sehemu iliyobaki ni kwa ajili ya mahusiano Yangu na yako. Kilicho kwa ajili Yangu ni roho yako. Sehemu nyingine ambayo ni kwa ajili yako ni vitendo vyako, na sehemu ya tatu iliyopo kwa ajili ya mahusiano baina yako na Yangu (Allah) ni uomabaji dua kwa upande wako na kutakabal hizo dua ni upande Wangu.
5. Ee Mwanaadam! Kuwa mnyenyekevu ili unijue Mimi. Mimi

## **Hadithi Qudsi**

ukinitaka utanipata kwa kuwa mpweke.

6. Ukae na njaa ili uweze kuniona Mimi.
7. Niaubudu ili uweze kunipata.
8. Uwe peke yako (tengana) na dunia ili ufile Kwangu.
9. Ee Mwanaadam! Wafalme watatupwa Motoni kutokana na udhalimu wao. Warabu kutokana na fahari ya kuwa mwarabu, wanavyuoni kutokana na uviwu, wafanya biashara kutokana na udanganyifu wao, wakulima kutokana na ujinga wao, wafanya ibada kutokana ushaufu wa kuonyesha ufahari wao, matajiri kutokana na kiburi chao, maskini kutokana na uzembe wao, wati-aji rangi nguo kutokana na ulaghai wao, wanaozuia Zaka kutokana na uzuiaji wa utoaji Zaka.

### **BASI YUKO WAPI MTAFUTAJI WA PEPO?**

## **SURA YA 28**

### **UWE UNAJALI FARADHI YAKO KUHUSU MUNGU WAKO**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

Enyi Mnaoamini! Mcheni Mwenyezi Mungu kikomo cha kumcha.  
Na wala msife ila mkiwa nyinyi ni Waislamu.

Ee Mwanaadam! Mfano wa amali bila maarifa ni mfano wa radi bila mvua.

Elimu bila vitendo ni mfano wa mti usio na matunda.

## **Hadithi Qudsi**

Elimu bila ucha-Mungu na unyenyekevu ni sawa ya mali isiyotolewa Zaka, chakula bila chumvi na kilimo juu ya jabali.

Mfano wa hekima mbele ya mpumbavu ni sawa na rubi na yakuti (vito) mbele ya wanyama.

Mfano wa nyoyo ngumu ni kama jiwe gumu majini. Mawaidha kwa mtu asiyetaka kusikilizaa ni sawa kupiga zumari mbele ya maiti makaburi.

Mfano wa kutoa sadaka kwa mali ya haramu sawa na mtu kuosha kinyesi kwa mkojo wake.

Swala bila kutoa Zaka ni mfano wa mwili bila roho.

Vitendo vyema bila toba ni sawa kama ujenzi bila msingi. Je! Wanafikiri wamesalimika dhidi ya adhabu ya Mwenyezi Mungu? Madhalimu hawatasalimika dhidi ya adhabu ya Allah (s.w.t.).

## **SURA YA 29**

### **NIKUMBUKE MIMI KWA DHATI NA KWA NIA**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

Ee Mwanaadam! Kadri moyo wako unavyoendekeza hii dunia basi mapenzi Yangu hutoweka moyoni mwako.

Bila Shaka Mimi Allah (s.w.t.) sitaruhusu mapenzi Yangu na mapenzi ya hii dunia yawe na makazi katika moyo mmoja.

Jitenge kwa ajili ya ibada Yangu.

## **Hadithi Qudsi**

Jiepushe na ria, hapo nitakuvisha mavazi ya mapenzi Yangu.

Elekea Kwangu na jipe muda wa kunikumbuka, hapo Nitakukumbuka mbele ya malaika Wangu.

Ee Mwanaadam! Ninyenyeknee Mimi (Allah) na Mimi nitakuzawadia fadhila zangu.

Nikumbuke Mimi kwa kupigana na nafsi yako. Mimi nitakukumbuka kwa kukutazama.

Nikumbuke hapa duniani katika uhai wako na Mimi nitakukumbuka wewe kaburini.

Nikumbuke katika hali ya ukwasi (utajiri) na afya njema. Mimi nitakukumbuka katika umaskini, dhiki na maradhi.

Nikumbuke Mimi kwa utii wa dhati na Mimi nitakukumbuka kwa msamaha.

Nikumbuke Mimi kwa kuwahurumia maskini, Mimi nitakukumbuka katika Pepo mahali pa kimbilio.

Nikumbuke kwa utumwa , Mimi nitakukumbuka kwa ulezzi.

Nikumbuke Mimi kwa kujisalimisha; Mimi nitakukumbuka kwa utukufu.

Nikumbuke Mimi kwa kulia (kuomba toba Kwangu kwa masikitiko) Mimi nitakukumbuka kwa kukuhurumia.

Nikumbuke kwa maneno (kwa kuomba dua Kwangu) Mimi nitakukumbuka kwa zawadi.

## **Hadithi Qudsi**

Nikumbuke Mimi kwa kutengana na dunia Mimi nitakukumbuka kwa uongofu wa Akhera.

Nikumbuke katika dhiki kuu na Mimi nitakukumbuka kwa wokovu kamilifu.

## **SURA YA 30**

**NIKUMBUKE MIMI KWA KUDUMU (KUOMBA TOBA KWA KULIA NA MASIKITIKO) NA MIMI ALLAH (S.W.T.) NITAKUKUMBUKA KWA KUKUHURUMIA**

**ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

Nikumbukeni Mimi nami nitawajibu.

Niombeni Mimi bila uzembe kwa (dhati na bidii) nami nitawajibu bila kuchelewa.

Niombeni Mimi kwa moyo safi (moyo uliotakasika na mapenzi), Mimi nitawatikia kwa kuwajalia hadhi kuu.

Nikumbukeni Mimi kwa moyo safi na kwa kuniogopa. Mimi Nitawaitikieni kwa kuwazawadia Pepo ambayo ni pahala pa kimbilio.

Niombeni kwa kuwa na khofu moyoni mwenu na matarajio, nami nitakujalieni mafanikio na kufanya mambo yenu kuwa sahali.

Niombeni kwa Majina Yangu Adhimu ya Kunitukuza Mimi Nitawatimizia matalaba yenu.

## **Hadithi Qudsi**

Niombeni katika nyumba ya kuhiliki (duniani) Mimi nitakujibu katika nyumba ya zawadi na kudumu milele.

Ee Mwanaadam! Hadi lini utaendela kusema Allah, Allah, wakati huo huo unafuga wengine moyoni mwako.

Ulimi wako unamkumbuka Allah (s.w.t.) lakini wewe huwaogopa wengine na kuwa na matumaini na mwengine asiyekuwa Allah (s.w.t.).

Laiti ungemjua Allah (s.w.t.) usingejali chochote ila Allah (s.w.t.).

Unafanya dhambi kwa kumuasi Allah lakini huombi msamaha kuto-ka kwa Allah (s.w.t.).

Kwa hakika kuomba msamaha na kuendelea kutenda maasi (wakati huo huo) ni toba ya uwongo. Allah (s.w.t.) Amesema ndani ya Kurani: Allah (s.w.t.) siye dhalimu kwa viumbe wake. (Kurani Tukufu (41:46).

## **SURA YA 31**

### **AKHERA PEPO YANGU: INAZIDI DHARAU**

#### **DUNIA**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Ee Mwanaadam! Kifo chako kinadhihaki matamanio yako.
2. Majaaliwa Yangu hudharau kifo chako.
3. Qadari Yangu (majaaliwa) hucheka mipangilio yako.

## **Hadithi Qudsi**

4. Akhera Yangu huidhihaki dunia yako.
5. Neema Zangu hudhihaki pupa yako. Kwa hakika riziki yako hujulikana: Imeshapangwa, ishaandikwa na kuhifadhiwa.
6. Kwa hivyo fanya haraka kwa ajili ya kifo chako kwa vitendo vyema kabla ya mauti haijakteka; kwa sababu hakuna mtu atawenza kuipatia riziki yako.
7. “Sisi Tumeshawagawanya riziki katika uhai wao duniani; na wengine kwa kuwatukuza (kwa kuwajaalia kwa wingi) kwa darja. Kwa hivyo baadhi yao huwashinda wengine na rehema waliojaaliwa na Allah (s.w.t.). Hao ni bora kuliko wanayokusanya mali.” (Quran Tukufu (43:42). Ee Mwana wa Adam! Dunia ni chungu kwa vipenzi Vyangu, lakini wao hutamani kukutana na Mimi. Na ni tamu kwa maadui Wangu, lakini wao huchukia kukutana na Mimi. Ee Mwana wa Adamu! Kifo kitakufikia tu hata kama unachukia. Kuwa na subra katika Amri za Allah (s.w.t.) kwa sababu wewe utafufuliwa. Basi mtakase kwa kumuhimidi Mola wako Mlezi wako: Kwa kukesha usiku na wakati nyota zinapotoweka.

## **SURA YA 32**

### **ANAYENITAFUTA MIMI (ALLAH) BASI ATANIPATA**

#### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Ee Mwanaadam! Wewe unapanga mipango yako na Mimi napanaga mipango Yangu; lakini hakuna kinachokuwa ila niliyopanga Mimi.
2. Yeyote atayejaribu kunifikia Mimi atanipata.

## **Hadithi Qudsi**

---

3. Yeyote atayenipata Mimi basi ananitaka.
4. Yeyote anayenitaka Mimi atanitafuta.
5. Yeyote atayenipata Mimi hunitumikia Mimi tu.
6. Yeyote anayenipata Mimi hunikumbuka Mimi tu.
7. Yeyote anayenitafuta Mimi, hunipata.
8. Yeyote anayenikumbuka Mimi, basi Mimi Humkumbuka kwa rehemba Yangu.
9. Ee Mwanaadam! Vitendo vyako havitakasiki bila kuonja vifo namna nne:
  - i) Kifo chekundu
  - ii) Kifo cha njano.
  - iii) Kifo cheusi.
  - iv) Kifo cheupe.

Kifo chekundu: Ni kuvumilia ukame na kujihini kuwadharau wengine.

Kifo njano: Ni njaa na dhiki.

Kifo cheusi: Ni kutotii matamanio ya ubinafsi. Kwa hivyo usitii matamanio, vingenevyo vitakupotosha kutoka njia ya Allah (s.w.t.).

Kifo cheupe ni kujitenga na dunia.

## **Hadithi Qudsi**

### **SURA YA 33**

#### **MIMI NAYAJUA YALIYOJIFICHA MOYONI MWAKO**

##### **ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Ee Mwanaadam! Lolote usemalo chochote utendacho kikiwa kichache na kingi Malaika Wangu wanakuona kila usiku na mchana ili waweke kumbukumbu.
2. Mbingu zinashuhudia ulichofanya.
3. Ardhi hii itakuwa shahidi kwa kila jambo utendalo juu yake.
4. Jua, mwezi na nyota ni mashahidi kwa cho chote utendacho au usemacho.
5. Lolote lililojificha moyoni mwako Mimi (Allah s.w.t.) hulielewa.
6. Usighafilike na nafsi yako kwa sababu katika mauti una kazi ngumu.
7. Bada ya muda mfupi tu wewe utaelekea kwenye kifo.
8. Chochote kibaya au chema ulichokipeleka kimehifadhiwa bila ya punguzo au nyongeza.
9. Utapata malipo ya kila ulichotenda.
10. Ee Mwanaadam! Vitu vya halali kamwe haviji ila kidogo kidogo, lakini vya haramu huja kama mafuriko. Yeyote aliyejitakasa maisha yake itatakasika dini yake.

## Hadithi Qudsi

### SURA YA 34

**EE MWANAADAM! USIDAGANYIKE NA KIMETO NA MVUTO WA DUNIA:**

**ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

Ee Mwanaadam! Usifurahike na mali yako; hiyo mali haitadumu daima.

Usihuzunike kwa sababu ya umaskini, huo sio mzigo wala hauku-fanywa wajibu.

Usikate tamaa kwa sababu ya mitihani; kwa hakika dhahabu hujaribiwa kwa kuyayushwa katika moto, vile vile muumini hupata majaribio kwa maafa (balaa).

Kwa hakika tajiri huheshimika duniani lakini hudhalilika Akhera; na maskini hudhalilika hapa duniani lakini kuheshimika kesho Akhera.

Kwa hakika Akhera ni ya mafanikio na ya milele.

Ewe Mwanaadamu ukimuona dhaifu amefungwa kwako zaidi ya siku tisa, basi sema: Najikinga kwa Mwenyezi Mungu dhidi ya ghadhabu ya Mwenyezi Mungu.

Ee Mwanaadam! Mali yote ni Yangu (Allah s.w.t.). Matajiri ni wawakilishi Wangu, na maskini wananiegomea. Yeyote aliye kuwa bakhili kwa wanaonitegomea basi Mimi nitamtia Jahannam na sitamjali.

## Hadithi Qudsi

Ee Mwanaadam! Mali yote Ni Yangu (Allah s.w.t.) na wewe ni kiumbe changu, mgeni ni mjumbe wangu na mukizua kutoa mali yangu kumpa mjumbe Wangu basi usitumai kupta Pepo Yangu na neema Yangu.

Ee Mwanaadam! Vitu vitatu vimefaradhishwa kwako. Zaka ya mali yako. Hurumia jamaa zako, na kumkirimu mgeni wako. Ikiwa hutatekeleza faradhi juu yako basi bila shaka nitakuzingira katika khofu na kukufanya kiigizo kwa binadamu.

Ee Mwanaadam! Kama hutawajali majirani zako kama unavyojali watoto wako Mimi sitakujali wewe. Mimi sitapokea amali yako na dua zako.

Ewe Mwanaadamu usimfanyie binadamu mwenzio kiburi, kwani mwanzo wako ni tone chafu la manii yatokayo kwa nguvu, hivi una-jua umetokea njia ipi? Umetokea njia ya mkojo kutoka katikati ya mifupa ya mgongo na kifua

Ee Mwanaadam! Kumbuka wakati utaposimama mbele Yangu hali ya kuwa dhalili!

Kwa hakika Mimi sighafiliki na siri zako hata punde na Mimi ni Mjuzi wa yaliyoko moyoni; hata mpepeso wa macho.

“Kwa hakika mimi Allah (s.w.t) Huelewa siri zilizo moyoni”  
(3:119)

## Hadithi Qudsi

### SURA YA 35

**KUWA NA HURUMA NA MKARIMU KWA WENGINE:**

**ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Ee Mwanaadam! Kuwa mkarimu: Kwa hakika Ukarimu unatokana na wema na yakini. Yakini inatokana na imani juu ya dini ya Allah (s.w.t.) na imani hutoka Peponi.
2. Ee Mwanaadam! Kuwa mwangalifu! Tahadhari! Usiwe bakhili. Kwa hakika ubakhili hutokana na kufuru na kufuru hutokana na Moto.
3. Ee Mwanaadam! Tahadhari na dua ya waliodhulumiwa kwa sababu hakuna kitu kinachoizua kufika kwangu. Lau mimi nisingekuwa mwenye kusamehe nisingempa Adam (a.s.) mitihani kwa dhambi na baadaye kumrudisha peponi.
4. Ee Mwanaadam! Ingekuwa Mimi sipendi kusamehe nisigewajaribu viumbe wangu kwa dhambi.
5. Ee Mwanaadam! Mimi Nimekujalia imani na usamehevlu bila kuniomba na kunililia. Basi viyi nitakufanya ubakhili wa Pepo na msamaha wakati wewe unaomba kwa unyenyekevu.
6. Ee mwanaadanu! Ikiwa kiumbe Wangu atashikamana na Mimi basi Mimi nitamwongoza.
7. Ikiwa yejote atanitegemea Mimi basi nitamtosheleza, na kama atamtegemea mwingine nisiyekuwa mimi, basi nitamkatia

## **Hadithi Qudsi**

mawasiliano ya mbinguni na ardhini.

8. Ikiwa ye yote atayemuamini mwingine isipokuwa mimi, basi Mimi nitamnyima fadhila za mbingu hapa duniani na Pepo kesho Akhera.
9. Ee mwanaadanu! Usikose Swala ya dhuhaa, kwa sababu vitu vyote vinavyoangazwa na jua humuombea yule anayeswali.
10. Ee mwanaadanu! Umedharau amri Zangu zote na umejizatiti kutenda dhambi. Basi nani Siku ya Kiyama atakukinga dhidi ya adhabu Yangu?

## **SURA YA 36**

**KAMA UPENDAVYO KWA AJILI YAKO, BASI UPENDE HIVYO HIVYO KWA AJILI YA WENGINE**

**ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:**

1. Ee mwanaadanu! Uwe na mwenendo mzuri na watu ili Mimi nikupende na nijaalie mapenzi yako katika miyo ya wacha-Mungu na nikusamehe dhambi zako.
2. Ee Mwanaadam! Weka mikono yako juu ya kichwa. Tafakari! Chochote unachopenda kwa ajili yako basi vivyo hivyo upende kwa ajili ya waislamu.
3. Ee Mwanaadam! Usihuzunike na cho chote unachokosa duniani na usifurahi kwa uliyopata duniani. Kwa hakika leo dunia ni yako

## **Hadithi Qudsi**

na kesho itakuwa ya mwingine.

4. Ee mwanaadanu! Hangaikia Akhera na iyache dunia, kwa sababu chembe kidogo kabisa cha Akhera ni bora kuliko vitu vyote duni-ani.
6. Ee mwanaadanu! Wewe unajibidisha kupata dunia wakati Akhera inakutafuta wewe. Ikiwa Mimi ningependa kuwajaalia dunia kwa mmoja wa watumishi Wangu basi ningewajaalia Mitume Wangu na wangewavuta watu kutii Amri Zangu.
7. Ee mwanaadanu! Matajiri wamekuwa wanyonge kutokana na kifo.
8. Wangapi waliokuwa wanacheka, mauti yamewafanya kuwa ni wenye kulia.
9. Viumbe Wangu wangapi niliowajaalia fadhila Zangu duniani lakini walivuka mipaka kwa kufanya maasi na kutonitii Mimi; mpaka kifo kikawateka na kuwatumbukiza katika Jahannam?
10. Viumbe Wangu wangapi ambao nimewajaribu kwa maafa na balaa lakini wamekuwa na subra. Hao wamefariki dunia na wameingia Peponi.

## Hadithi Qudsi

### SURA YA 37

#### USIJIONYESHJE

#### ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:

1. Ee mwanaadanu! Wewe huanza siku kwa fadhila mbili kubwa: Wewe huelewi ni ipi kubwa zaidi kuliko nyingine: Maasi yako yamefichika mbele ya macho ya watu au sifa njema unayopata kutoka kwa watu?
2. Ikiwa watu watajua habari zako kama ninavyoolewa Mimi hatakuwa hata kiumbe Wangu mmoja atakayekusalimia. Takasa amali yako kutokana na riya kwani wewe ni mja dhalili wa Mola ni Mtukufu.
3. Zidisha akiba yako (vitendo vyema). Kwa hakika wewe ni msafiri unayeelekea Akhera! Na lazima kila msafiri kuwa na akiba ya kutosha.
4. Ee mwanaadanu! Hazina Yangu kamwe haiishi. Mikono yangu daima imekunjuka kwa kutoa. (Daima i wazi kuzawadia).
5. Kwa kadiri utakavyotoa ndivyo nitakavyokupa, na kwa kadiri utakavyonyima ndivyo nitakavyokunyima.
6. Utapozuia kutumia katika njia yangu basi nitazuia fadhila zangu.
7. Ee mwanaadanu! Kuogopa ufukara ni kutomuamini Allah Aliyetukuka. Kwa sababu Kutomuamini (Allah) ni udhihirisho

## Hadithi Qudsi

wa dharau yako kwa maskini.

8. Ee mwanaadanu! Wale wanaopupia kwa ajili ya riziki yao, kwa uhakika hawakuamini Kitabu Changu (Kur'an). Na asiyewaamini Mitume Wangu basi kakanusha utawala Wangu, na yejote anayekanusha utawala Wangu bila shaka nitamtumbukiza katika janga hapa duniani.

## SURA YA 38

### EE MWANADAMU! WEWE NI KIUMBE MDHOOFU NA MIMI BWANA MTUKUFU NA MWENYE UWEZO WOTE

#### ALLAH (S.W.T.) ANASEMA:

1. Ee mwanaadanu! Jibiidishe ili ulimi wako na moyo wako vikubaliane. ulimi ukubaliane na vitendo vyako. Takasa vitendo vyako kwa kuwa na mwenendo kwa ajili ya kupata ridhaa Yangu.
2. Bila shaka ulimi wa mnafiki haukubaliani na moyo wake; na ulimi wake haukubaliani na vitendo vyake; na vitendo vyake vinakuwa kwa ajili ya mwingine asiyekuwa Allah (s.w.t.).
3. Ee Mwanaadam! Lolote unalolisema kwa kinywa chako, lolote unaloliona kwa macho yako, hatua yoyote unayochukua, kuna malaika wawili ambao huweka kumbukumbu kwa ajili yako na dhidi yako.
4. Ee mwanaadanu! Mimi Sikuwaumba kwa ajili ya kukusanya mali kwa ajili yako au kwa ajili ya wengine; lakini nimewaumba ili mniabudu Mimi. Kuweni wenyenekewu na kunishukuru

## Hadithi Qudsi

---

kwa wingi, kunihimidi na kutukuza Utukufu Wangu kutwa na kuchwa. Kwa hakika riziki zenu zimeshapangwa. Mlafi hunyimwa na mchoyo hushutumiwa. Hasidi huhuzunika. Anayetoa majaribio yu hai daima na milele.

5. Ee mwanaadanu! Nitumikie Mimi. Mimi Huwapenda wanaonitumikia. Kwa hakika wewe ni mtumwa uliopoteza uwezo wote.
6. Ikiwa ndugu zako watanusa harufu ya dhambi zako, kamwe hawatakaa karibu nawe. Dhambi zako kila siku huongezeka na maisha yako hufupika. Usipoteze maisha yako katika uzembe. Ikiwa unataka nyongeza basi kuwa sahibu na wakarimu. Jipaties kimbilio kwa kutengana na hii dunia na ishi kwa kuwa na uhussiano na mafukara.
7. Ee mwanaadanu! Yule ambaye safina yake imeteketea baharini na hutegemea kipande cha mbao kinachoelea, matatizo na mushkeli yake hayako makubwa kuliko yako: kwa sababu unaelewa dhambi zako.
8. Ee Mwanaadam! Mimi huwa karibu na wewe kwa kukujaalia ukwasi na kuficha dhambi zako. Na wewe unanifanya Mimi Allah (s.w.t.) adui wako kutokana na ukaidi wa kutonitii, kuen-dekeza hii dunia na kuangamiza Akhera Yako.
9. Ee mwanaadanu! Ikiwa hutafanya usuhuba na watu waliofaulu wema basi lini utafafulu?
10. Ee mwanaadanu! (Nabi Musa a.s.) mwana wa Imran! Sikiliza kwa umakini ninayosema: Hakuna mtu anaweza kupata fursa kumfikiria Allah (Mimi) ila yule ambaye watu wanosalimika dhidi ya madahara yake. Yaani wanosalimika dhidi ya ukandamizi, hila, umbeya, udaku, usengenyaji, dhulma, husda, na

## Hadithi Qudsi

madhara, katika hali ya dhahiri na siri.

11. Ewe Musa! Waambie wale wakandamizaji kwamba wasinikumbuke Mimi, kwa sababu Mimi siwakumbuki na kama niki-wakumbuka basi huwalaani tu. Kwa hivyo kila mtu yupo huru kuniamini au kutoniamini.

## SURA YA 39

### HII DUNIA NI BURUDANI NA MCHEZO

#### ALLAH (S.W.T) ANASEMA::

1. Ee mwanaadanu! Usikaidi Amri Zangu na wala usiombe msama-ha.
2. Ee mwanaadanu! Niombe kwa kuninyenyekaa katika ibada Yangu. Vingenevyo, nitajaza moyo wako ufukara, mikono yako matatizo, mwili wako mateso, kifua chako huzuni. Sitapokea dua zako na Nitageuza dunia iwe ngumu dhidi yako na nitaipunguza riziki yako.
3. Ee mwanaadanu! Mimi huridhika na ibada yako ya kila siku, kwa hivyo wewe ridhika na riziki yako siku bada ya siku.
4. Ee mwanaadanu! Nenda Taratibu! Kwa hakika riziki yako imepangwa. Mlafi hunyimwa, mwenye husda hudhalilika. Fadhila za dunia hazidumu.
5. Ee mwanaadanu! Tengeneza jahazi yako madhbuti. Kwa hakika bahari ina kina kikuu. Ongeza akiba yako kwa sababu safari ni ndefu na ngumu.

## **Hadithi Qudsi**

6. Ewe Musa! Bila shaka viumbe huwa na uwezo wa kutenda viten-do mpaka wanapotekwa na kifo. Badaye hujutia kwa dhambi na maovu walijotenda. Hapo tena hutamani kurudi duniani na kuten-da mema. (Kur'an Tukufu (32:12).
7. Naapa kwa uwezo na heshima Yangu! Sitamrudisha hata mmoja wao.
8. Ee Musa! Yeyote anayeniridhisha kwa kuniogopa na Mimi nita-mpa jazaa yake ambayo ni Pepo.
9. Ee Musa! Maisha ya hapa duniani ni burdani na kiburdisho tu!, pambo na majisifu (baina ya watu)" (Kurani Tukufu: 57:20).
10. Kwa ajili ya muumini hakuna kitu hapa duniani ila ibada, huzu-ni na matatizo. Pepo iko kwa ajili yake.

Ee Musa! Siku ya Hukumu ni ngumu! Hofia sana siku hiyo wakati baba hatakuwa na msada kwa mwana, na wala mtoto hatakuwa na msada wo wote kwa baba yake. (Kuran Tukufu (31:33).

11. Wangapi wameachana na makazi yao hapa duniani kuhama makazi yao yaliyohiliki na kuelekea Akhera kwa furaha na shukrani?
12. Wangapi matajiri wameacha mali yao hapa duniani na kuelekea Akhera peke yao, wakiwa wanyonge na kujutia vitendo vyao?
13. Hao wanahodhi mali kwa ajili ya warithi wao, siku ya hukumu watapata adhabu kali na wataendelea kupata hiyo adhabu mful-ulizo kutohana na ustahiki wao!

**Tamat. Alhamdu-Lillahi-Rabuul-Alameen.**

## Hadithi Qudsi

---

## Hadithi Qudsi

---

## Hadithi Qudsi

---